

HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri)

ANUANI: "MKURUGENZI"

Simu Na. -----

Fax Na. -----



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),

S.L.P. 22,

Mahenge/Ulanga.

Website: ww.ulangadc.go.tz

Barua pepe: ded@ulangadc.go.tz

KUMB. NA. UDC/ADM/B. 10/12/189

28/05/2020

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga anapenda kuwatangazia waombaji wote walioomba kazi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji daraja

la III kuwa usaili utafanyika kuanzia tarehe **08 HADI 09 JUNI 2020 saa 1.00** asubuhi katika shule ya msingi Mahenge. Aidha usaili wa mchujo (Written Interview) utafanyika tarehe **08 Juni, 2020**, na wasailiwa watakaofaulu ndio watakaochaguliwa kuendelea na usaili wa mahojiano (Oral Interview) tarehe **09 Juni, 2020** katika ukumbi wa Halmashauri (Pauline Hall) siku ya Jumanne kuanzia saa 1:00 Asubuhi.

Orodha ya waombaji walioitwa kwenye usaili ni kama inavyoonekana hapo chini, kwa waombaji ambao majina yao hayakuonekana katika orodha hiyo watambue kuwa maombi yao hayajakidhi sifa kwa mujibu wa nafasi zilizotangazwa, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya anawashukuru kwa kuleta maombi ya kazi na wasisite kutuma maombi tena pindi Halmashauri itakapotangaza nafasi za kazi ambazo zitaendana na sifa walizonazo.

Waombaji wote walioitwa kwenye usaili wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo;

- i. Wasailiwa wafike na Vyeti Halisi (Original) vya Taaluma, Kuzaliwa Vyeti vya Shule na Kitambulisho.
- ii. Vitambulisho vitakavyokubaliwa ni pamoja na Kitambulisho cha Uraia, kitambulisho cha kupiga kura, Leseni ya udereva au Pasi ya Kusafiria.
- iii. Kwa waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe Vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU , NACTE na NECTA);
- iv. Msailiwa anayekuja kufanya usaili atajigharamia mwenyewe.
- v. Msailiwa anatakiwa kuzingatia tarehe, muda na eneo la usaili

